HAKIARDHI

# ARDHI NI UHAI

ISSN NO. 0856-9495 TOLEO LA 1 Juni 2004

YALIYOMO


| | |
|---|---|
| Njama za Kikabaila | 1 |
| Tahariri | 2 |
| Hanang: Kwa ajili yetu | 4 |
| Uhaba palipo na Tele | 5 |
| Bunga Bongo;Uthamanishaji wa Ardhi | 6 |
| Wahoji uporaji wa ardhi | 9 |
| Maoni ya wananchi | 10 |
| Machapisho | 11 |


## NUKUU YA LEO

"Wakati watu wengi watakapokubali njia ambayo itawawezesha wachache kumiliki kitu ambacho kwa kweli ni zawadi ya mungu kwa watu wote,watakuwa wakiukubali utumwa kwa hiari yao wenyewe."

J.K. Nyerere

Sheria ya Marekebisho ya Sheria za Ardhi ya 2004

## NJAMA ZA KIKABAILA DHIDI YA WANYONGE?

*Prof. I.G. Shivji*

Mwezi Februari mwaka huu, Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania lilipitisha Sheria ya Marekebisho ya Sheria ya Ardhi ya Mwaka 2004. Sheria ya Marekebisho 2004 inaleta mabadiliko makuu mawili kwa sheria za ardhi za mwaka 1999. Badiliko la kwanza linahusiana na uuzaji wa ardhi isiyoendelezwa (yaani ardhi tupu) na badiliko la pili ni la ardhi kutumika kama dhamana ya mikopo. Msukumo wa mabadiliko haya, hususan lile linalohusu rehani ya ardhi kwa ajili ya mikopo, ni hoja ya kumrahisishia mkopeshaji kuchukuwa mali iliyowekwa rehani pindi mkopaji anaposhindwa kurejesha mkopo. Jambo moja hapa ni dhahiri, sheria hii inavyosomeka ni kama vile ilani ya mkopeshaji, iliyoandikwa na mwanasheria wa Benki - ambaye ana maslahi makubwa na mabadiliko haya. Kwa ujumla nisingependa kuongelea kipengele hiki kwa undani zaidi kwani watu wengine wameshakijadili vya kutosha.

Ninalopenda kuongelea zaidi ni suala la uuzwaji wa ardhi tupu. Jambo kubwa na muhimu kuzingatia ni kuwa kwa mara ya kwanza, katika historia ya mfumo wa umilikaji ardhi Tanzania, Sheria imeruhusu uuzaji wa ardhi isiyo endelezwa (ardhi tupu). Ikumbukwe, hapo awali, kabla ya marekebisho haya, mfumo wa umilikaji ardhi ulikuwa ni wa aina kuu mbili: yaani *umiliki wa adhi wa kimila* na *umiliki wa ardhi kwa hati*. Aina zote mbili zilijengwa juu ya misingi mikuu miwili: Mosi, ardhi ni kwa ajili ya matumizi na pili, uhakika wa kuendelea kutumia ardhi ulitokana na matumizi. Kwa mfano katika umiliki wa ardhi kimila hakukuwa na dhana ya mtu kumiliki ardhi tupu. Hii ni kwa sababu ardhi tupu ilichukuliwa kama zawadi toka kwa mababu (Mungu). Kwa mantiki hii mtu alitambuliwa kukalia ardhi kama tu alikuwa akiitumia. Haki hii, kwa mujibu wa taratibu zake, ilidumu kama tu anayeikalia anaendelea kuitumia. Kama mtumiaji wa ardhi ataacha kuitumia ardhi kwa kipindi kinachokubalika ardhi hiyo hubaki kuwa mali ya jamii kwa ajili ya kugawiwa mtu/watu wengine wanaohitaji kuitumia.



*Prof. Issa Shivji akitoa mada katika moja ya warsha zinazoandaliwa na HAKIARDHI*

Mfumo wa kumiliki ardhi ulioanzishwa na Sheria ya Ardhi ya mwaka 1923 ulishabihiana kwa karibu sana na mifumo ya kimila.

Endelea Uk.3

**Ardhi ni Uhai** ni jarida la HAKIARDHI ambalo hutolewa mara tatu kwa mwaka. Kusudi kubwa ni kuwapa wadau wa Taasisi hii taarifa mbalimbali zinazohusiana na mambo ya ardhi.

**Mchapishaji**
HAKIARDHI

**Mhariri**
Agripina Habicht

**Bodi ya Wahariri**
Ng'wanza Kamata - M/Kiti
Agripina Habicht - Mhariri
Abdallah Matata - Mjumbe
Rehema Mfaume - Mjumbe

**Mchapaji**
Ecoprint Ltd.

# UJUMBE WA BODI KWA WASOMAJI

Wasomaji wa jarida hili wanakaribishwa kutoa michango yao kwa kuuliza maswali au kwa kuandika makala. Maswali, Maoni na Makala (zisizozidi kurasa tatu) zitumwe kwa Mhariri kupitia anuani ifuatayo:

Mhariri:
Ardhi ni Uhai
S.L.P. 75885
Dar es Salaam

Email:
editor@hakiardhi.org

# TAHARIRI

Hivi karibuni Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania lilipitisha muswada wa Marekebisho ya Sheria za Ardhi za Mwaka 1999. Chimbuko na msukumo wa marekebisho hayo lilikuwa ni matakwa na malalamiko ya Mabenki na wahisani kuwa vipengele kadhaa vya Muswada wa Sheria ya Ardhi vilikuwa vinapingana na sera zao za ukopeshaji na azma ya Serikali ya kuvutia wawekezaji katika kilimo na kupambana na Umasikini. Aidha Mabenki yalidai kuwa Sheria ilikuwa haiwapi hamasa ya wao kuwakopesha wakopaji wadogo ambao wangetumia ardhi kama dhamana kwa vile wakopaji wa aina hiyo walilindwa mno na Sheria.

Mapendekezo haya ya Mabenki yalizua mjadala ambapo hoja mbali mbali za wachambuzi wa masuala ya ardhi zilibaini kuwa Serikali ilikuwa na mpango, kutokana na shinikizo la wafadhili, kubinafsisha ardhi. Hoja hii ilipingwa vikali na Serikali. Katikati ya mjadala huu Serikali iliuhakikishia umma kuwa ardhi itaendelea kuwa mali ya umma na kwa upande mwingine ilikuwa ikiwahakikishia wawekezaji kuwa Sheria itarekebishwa ili kutoa mazingira bora kwao kuja kuwekeza kwenye ardhi.

Ni dhahiri kuwa matokeo ya Sheria ya Marekebisho ya Sheria ya Ardhi ya 2004 yanatoa fursa ya umiliki wa ardhi huria bila Sheria kutamka hivyo. Ni dhahiri pia kuwa hoja ya mikopo na kuondoa umasikini imetumiwa na wenye uchu wa kuwa makabaila kujijengea mazingira ya kisheria ya kufikia azma hiyo. Kwa mwelekeo huu nini hatma ya ardhi ya wamiliki na watumiaji wadogo na masikini wa vijijini?

Ikumbukwe kuwa katika maeneo mengi vijijini ardhi ya wananchi imekuwa ikiporwa kwa njia za ulaghai, upindaji wa Sheria au vitisho. Aghalabu uporaji wa aina hii ulivihusisha vyombo na ngazi mbalimbali za dola ambavyo vilifanya hivyo kwa niaba ya makampuni na watu binafsi wenye fedha au nafasi za kisiasa. Ushahidi wa vitendo hivi ni pamoja na ule uliokusanywa na Tume ya Rais ya Uchunguzi wa Masuala ya Ardhi juu ya malalamiko ya wananchi dhidi ya uporaji wa aina hii. Sheria ya Marekebisho ya Sheria ya Ardhi ya Mwaka 2004 inahalalisha vitendo hivi. Kwa kuruhusu ardhi tupu kuuzwa Sheria inatoa fursa kwa wenye uwezo wa kifedha kujilimbikizia ardhi na kisha kuiuza kwa bei ya juu hapo baadaye. Mazingira yanayoanzishwa na Sheria hii ni hatari kwa mustakabali wa wakulima wadogowadogo na wafugaji vijijini.

Aidha kwa kutarajia wakulima kubadilisha kilimo chao, kuboresha maisha yao na kuondokana na umasikini kwa njia ya kukopa toka kwenye mabenki ya biashara ni kukwepa ukweli kuwa i) Hakuna kokote barani Afrika ambako mabenki ya Kibiashara yamekuwa tayari kutoa mikopo kwa wakulima wadogo wadogo, na ii) si kawaida kwa mkulima kukopa na kuwekeza ardhi kama rehani. Ipo mifano mingi ya kihistoria inayoonesha kuwa wakulima waweza kukopeshwa pembejeo na zana za kilimo. Njia nyepesi na rahisi inayofahamika, ya kuwawezesha wakulima kukopa na kurejesha kwa uhakika ni kupitia ushirika wao. Hali kadhalika Serikali haina budi kuweka taratibu, sera na sheria zitakazoyataka mabenki, hususan yale ya wakopaji wadogo, kutoa mikopo kwa wakulima wadogo, na Serikali ikiwa kama mdhamini mkuu. Kwa kifupi, zipo njia mbadala na mwafaka za kutoa mikopo kwa wakulima bila kulazimisha wakulima kulazimika kutumia ardhi yao kama rehani, jambo ambalo linaashiria kuongeza kwa kasi ya ufukarishaji miongoni mwa wakulima watakaoshawishika ama kuuza au kuwekeza ardhi zao kama rehani kwa ajili ya mikopo.

Tanzania, kwa miaka mingi ijayo itaendelea kuwa nchi ya wakulima na wafugaji wadogo wadogo. Mabadiliko yenye uhakika na endelevu katika uchumi ni yale yatakayojengwa juu ya nguvu kazi ya wana vijiji, na rasilimali yao kuu - ardhi. Kinyume chake, sehemu ndogo ya watanzania yaweza 'kupaa' na wimbi la utandawazi, na kuwaacha asilimia 80 au zaidi ya watanzania wakiwa hata hawawezi kutambaa. Endapo mustakabali wetu utategemea wapaaji hawa, si vigumu kubaini nini yatakuwa matokeo yake.

Jambo muhimu ni kuwahakikishia wakulima miliki ya ardhi yao na kutafuta mbinu endelevu kwa ajili ya maendeleo ya shughuli zao juu ya ardhi bila kuwapora. Haya yanawezekana kama hatutatanguliza tamaa za kikabaila.

# NJAMA ZA KIKABAILA

*Inatoka uk. 1*

Chini ya mfumo huu mtu alipewa haki ya kumiliki ardhi kwa kipindi cha hadi miaka 99. Haki ya kumiliki ardhi ilimaanisha haki ya kutumia na kukalia ardhi na yeyote aliyepata haki hiyo alipewa pia masharti ya kuiendeleza. Kama mtu angeshindwa kuiendeleza ardhi hiyo alinyang'anywa - kwa maana kuwa alipoteza uhalali na haki juu ya ardhi.

Haki hii ya kukalia na kutumia ardhi iliweza kuuzwa, lakini hilo liliwezekana kwa idhini ya Kamishna wa Ardhi. Chini ya mfumo wa aina hii Kamishna wa ardhi, kinadharia, asingeruhusu ardhi tupu kuuzwa. Kwa hivyo mtu yeyote ambaye angejaribu kuuza ardhi tupu angekuwa amekiuka masharti ya kuiendeleza na hivyo kunyanganywa. Kilichokuwa kinauzwa, katika kuhamisha umiliki, ni yale maendelezo yaliyofanywa katika ardhi (mathalani nyumba, mazao, n.k). Kimsingi, mfumo huu umeendelea kuwepo katika sheria mpya za ardhi za mwaka 1999. Mathalani, kifungu kidogo cha 8 cha kifungu cha 37 cha Sheria ya Ardhi ya 1999 kilimzuia kabisa Kamishna wa ardhi kuidhinisha uuzaji wa ardhi isiyo na maendelezo kwa vile ardhi tupu ilitambulika kutokuwa na thamani. Kifungu kidogo cha 9 kilibatilisha (void ab initio) kabisa uuzaji wa ardhi tupu hivyo mnunuzi asingepata faida yoyote kutokana na ardhi hiyo tupu.

Kutokana na marekebisho yaliyofanywa na Sheria ya Marekebisho 2004 vifungu vidogo vya 8 na 9 vya kifungu cha 37 sasa vimefutwa. Badala ya vifungu hivyo kuna vifungu vipya. Kwa mujibu wa vifungu hivyo vipya Kamishna wa ardhi ameruhusiwa kuidhinisha uuzaji wa ardhi tupu endapo tu uuzaji huo unazingatia masharti yaliyopo kama yalivyoainishwa katika kifungu kidogo cha 9 cha Sheria ya Marekebisho 2004.

Kwa mujibu wa kifungu hiki, mauzo sharti yafanywe kwa raia wa Tanzania. Hata hivyo muuzaji anaweza kuwa mtu yeyote, raia ama asiye raia, ingawa kiutendaji si rahisi kwa mtu asiye raia wa Tanzania kumiliki ardhi tupu. Kwa upande mwingine raia anaweza kuwa na ardhi tupu anayoimiliki ama kwa miliki ya kimila ama miliki ya hati. Kimsingi sheria hii imeruhusu uuzaji wa ardhi tupu miongoni mwa raia. Kwa vile mnunuzi ni raia Kamishna wa ardhi sharti aruhusu uuzaji wa ardhi kwa kuzingatia misingi ifuatayo:

**I Pale mnunuzi atakapokubali masharti ya kuiendeleza ardhi.**

Hii ina maana kwamba mwanakijiji au mmiliki wa ardhi kwa hati, wa tabaka la kati, aishiye mjini ambaye ameshindwa kuendeleza ardhi yake anaweza kumuuzia raia mwenzake mwenye kipato cha juu anayeweza kuiendeleza. Watu wenye uwezo na nafasi ya kujipatia hati kutoka serikalini ambao hata hivyo hawako tayari kuitumia ardhi hiyo watapata fursa ya kuiuza kwa mtu/watu wengine.

> *Katika makoloni ya walowezi waafrika walipoteza ardhi yao kwa walowezi (wazungu) ambao walitumia nguvu za dola kuwapora waafrika ardhi yao. Huo ulikuwa ni wakati wa ukoloni na dola iliyotumika ilikuwa ni ya kikoloni. Je haitakuwa jambo la kustaajabisha pale watanzania watakapopoteza ardhi yao kwa njia ya masoko yaliyoanzishwa na serikali yao wenyewe?*

**II Pale uuzaji unapofanywa ili kuingia ubia kwa kusudi la kutimiza sharti la kuiendeleza ardhi.**

Hii inatofautiana na msingi nilioutaja hapo juu ingawa kwa sasa wanasiasa wameamua kuutumia mtindo huu kuingia katika ubia. Hii pia ni ndoto ya watu wa tabaka la kati (wenye tamaa za kuwa makabaila) ambao hawana mtaji lakini kwa kufahamiana na wanasiasa wanaweza kupata ardhi na kuitumia kuingia ubia. Lakini anayeingia ubia huo ni lazima pia awe raia, ingawa katika mfumo wa sasa wa kuundwa kwa makampuni uchwara, wanaoitwa wabia na ambao ndio wenye nguvu katika ubia huo, wanaweza pia kuwa sio raia.

Kwa vyovyote vile, wazo lililopo ni kuanzisha soko la ardhi. Lakini ni wazi kuwa soko ni njia ya kukuza mahusiano yasiyo sawa. Kwa mfano huu, bila shaka watu wajanja wa mijini na watu wenye uhusiano mzuri kisiasa, wataomba kugawiwa ardhi na kuiuza kwa raia matajiri. Na pili ni kwamba wanavijiji maskini watashawishika kuuza ardhi yao kwa matajiri na wao kubaki kuwa watwana.

Tunaelekea kwenye hali ile ambayo ilihofiwa na Mwalimu Nyerere mnamo mwaka 1958 alipoandika makala iitwayo Mali ya Taifa. Mwalimu alisema:

**"Katika nchi kama yetu, ambamo waafrika ni maskini na wageni ni matajiri, kuna uwezekano mkubwa kwamba Mwafrika akiruhusiwa kuiuza ardhi, katika miaka themanini au mia ijayo, ardhi yote ya Tanganyika itamilikiwa na matajiri wageni, na wenyeji watakuwa watwana. Lakini hata kama wageni wasingekuwa matajiri, litaibuka tabaka la Watanganyika matajiri na wajanja. Tukiruhusu ardhi iuzwe kama Kanzu, katika muda mchache, kutakuwa na kundi dogo la Waafrika wakiwa na ardhi na walio wengi watakuwa watwana" Mwl. J. K. Nyerere, 1958**

Mabadiliko yaliyofanywa yameleta misingi mipya ya mfumo wa umilikaji ardhi nchini. Ukweli ni kwamba yameanzisha utaratibu wa *miliki huria* (freehold) ya ardhi japo katika vitabu vya sheria unaendelea kujulikana kwa kivuli cha *ardhi ni mali ya umma*. Ninadiriki kusema hili kwa sababu ya sifa kuu za *miliki huria ya ardhi*. Mfumo wa *Miliki huria ya ardhi* unazo sifa kuu mbili: Kwanza, mmiliki wa ardhi ni mtu binafsi na pili ni kwamba anamiliki bila ukomo. Chini ya mfumo wa umiliki uliokuwepo kabla ya marekebisho haya umiliki wa ardhi ulikuwa ni wa Dola. Lakini sasa sheria inaruhusu mtu binafsi kumiliki ardhi. Kwa mantiki hii ukomo wa kumiliki ardhi uliopo kisheria hauna maana yoyote kwa vile sheria inaanzisha, bila kutamka, umiliki usio na kikomo umiliki wa milele.

Aidha yote yanayozungumzwa juu ya ardhi kuendelea kuwa ni "mali ya umma" hayana maana. Kwa mabadiliko haya wafadhili na Taasisi za fedha za kimataifa wamepata walichokuwa wanakihitaji kwa muda mrefu. Ardhi imegeuzwa kuwa bidhaa.

Swali lililo mbele yetu ni kwamba nini yatakuwa madhara ya uamuzi huu kwa maisha na ustawi wa wananchi zaidi ya asilimia 80 wanaotegemea ardhi?

# HANANG : KWA AJILI YETU NA WATOTO WETU

Ni wakati mgumu kimaisha kwa wakazi wengi wa vijiji vilivyo jirani au kuzunguka mashamba ya Ngano ya NAFCO wilayani Hanang Mkoa wa Manyara. Ni wakati wa njaa, wananchi hawana uhakika wa chakula na wanahaha huku na kule kukitafuta. Shughuli nyingi zimeahirishwa na pengine hazifikiriwi kabisa kwa vile nguvu na fikra zote zimeelekezwa katika kutafuta chakula kwa ajili ya kuganga njaa. Nyakati kama hizi zimajaa mahangaiko na wasiwasi mwingi wa nini kitatokea kesho, endapo leo itapita salama.


Pamoja na hali hii ngumu ya kimaisha wakazi wengi wa wilaya ya Hanang, hususan vijiji vya Ming'enyi, Gehandu, Dang'aida, Gawidu, Mulbadaw, Bassotu, Laghanga ambavyo vipo jirani na Mashamba ya Ngano ya NAFCO, wanakumbuka vilivyo historia za maisha yao. Moja ya kumbukizi hizo ni ile inayohusiana na kuondolewa kwao kwa nguvu kutoka katika ardhi yao ili kupisha kilimo cha mashamba makubwa ya ngano chini ya Shirika la Chakula la Taifa (NAFCO). Kumbukizi hizi zimejaa machungu ya mateso, udhalilishaji, dhuluma, ukandamizaji na mateso makubwa. Mbali ya kumbukizi za yaliyowasibu wakati wa kunyang'anywa ardhi yao, wengi hasa kina mama, wanakumbuka jinsi walivyoteswa na kudhalilishwa hata baada ya wao kulazimika kuondoka kwenye ardhi yao bila ridhaa yao.

Akikumbuka yaliyowasibu hapo nyuma mwanamke mmoja wa kijiji cha Dang'aida alisema "Wakati wa njaa kama huu tuliona ngano ikivunwa na kupakiwa kwenye malori kupelekwa kwa matajiri mjini Arusha. Hakuna aliyejali kama pia tulihitaji chakula na hakuna aliyejali angalau kupunguza bei ya ngano ili nasi tumudu kuinunua na kuganga njaa zetu". Masikitiko ya mwanamke huyu yanatokana na hali halisi ya mahusiano kati ya NAFCO katika enzi za 'mafanikio' yake na wananchi waliokuwa wakiishi jirani au pembezoni mwake. Kwa mujibu wa mama huyu mahusiano siyo tu yalikuwa mabaya na yenye mateso kwao bali pia kuwepo kwa NAFCO hakukuwa na manufaa yoyote miongoni mwao.




*Wanawake wa Basotu, wilaya ya Hanang baada ya kutoka kwenye mijadala ya vikundi. Kushoto ni Navaya Ndaskoy na katikati ni Joackim Mwami wa HAKIARDHI*

Pamoja na kutambua ubaya wa mahusiano kati ya NAFCO na wananchi njaa ilipowazidi walidiriki kuingia kwenye mashamba ya NAFCO. "Tulikuwa tukienda kuokota punje za ngano mara baada ya NAFCO kuvuna ngano yao", alieleza mwanamke mwingine, "lakini tuliishia kutandikwa viboko na kunyang'anywa punje zetu za ngano tulizookota", alimalizia kwa kumbukizi. Hadithi za kina mama wengi katika eneo hili ni za kusikitisha kwa vile si tu walinyang'wanywa ngano waliyookota punje moja moja kwa kupinda migongo yao bali pia walipigwa na kudhalilishwa. Kwa mantiki ya kawaida haya yasingestahili kutendewa wananchi na shirika la umma ilhali wao ni sehemu ya umma.



*Na Ng'wanza Kamata*

Yaliyopita si ndwele, walisema waswahili. NAFCO imefilisika na kwa karibu mwongo mmoja sasa sehemu kubwa ya ardhi iliyo chini ya NAFCO wilayani Hanang haitumiki kwa kilimo cha ngano. Serikali kupitia Kamati ya kurekebisha Mashirika ya Umma (PRS) imeyaweka mashamba haya chini ya mfilisi ikiwa ni hatua za mwanzo za kuyabinafsisha au kuyapangisha. Je, katika hatua hizi maamuzi na hatua za serikali zitaganga yaliyopo na yajayo au zitaibua upya hisia na kutonesha majeraha ya wakazi wa maeneo waishio jirani au kuzunguka mashamba ya NAFCO? Maamuzi na hatua za awali za serikali kutwaa ardhi ya wananchi kwa ajili ya mashamba haya zilisababisha majeraha makubwa miongoni mwao na baadhi ya majeraha hayajapona kabisa. Kuna haja ya kutibu kabisa majeraha haya.

Wananchi wenyewe, wake kwa waume, wanapendekeza kushirikishwa katika hatua zote zinazohusu uamuzi wowote mpya juu ya ardhi yao. Wanadai kuwa awali walipoondolewa kwa nguvu walitengwa na kulazimishwa kuondoka pasipo haki. Wengi wa wakazi wa maeneo kuzunguka mashamba ya NAFCO ni wakulima na wafugaji. Na tatizo lao la kudumu, ukiacha la njaa ambalo hutokea na kupotea

Endelea Uk. 9

# UHABA PALIPO NA TELE SIKU KUMI MIONGONI MWA WASIO NA ARDHI



Na Immanuel Mvulla

"Hakuna mwanakijiji aliyetoa ushahidi anayeweza kuonekana kuwa anamiliki ardhi kimila, kwa vile hakuna aliyeonesha au anayejaribu kunena kwa uthabiti kuwa ni mzawa; Baraza la kijiji cha Mulbadaw halikumiliki ardhi yeyote kwa sababu hapakuwa na ushahidi ulioonesha kwamba waliwahi kugawiwa ardhi na Baraza la Maendeleo la Wilaya; ukweli kwamba Baraza la kijiji lilirithi shughuli za kitawala za lile lililotangulia ambalo halikutambuliwa, haulipatii mamlaka yeyote Baraza hilo juu ya ardhi hiyo; kwa vile wanakijiji walikuwa wanamiliki kisheria kipande kwa ruhusa ya mrufani, walikuwa wanamiliki kisheria ardhi hiyo kwa kibali, hivyo wanaweza wakadai malipo kwa uharibifu wowote wa mali uliofanywa na mrufani" *(tafsiri binafsi)*

Nilipata kuisoma hukumu hii miaka miwili iliyopita wakati nikisoma kozi ya Sheria za Ardhi. Hii ilikuwa hukumu katika kesi ya Shirika la Kilimo na Chakula la Taifa (NAFCO) dhidi ya Baraza la Kijiji cha Mulbadaw. (National Agricultural and Food Corporation Vs. Mulbadaw Village Council CA 1985 (TLR) 88). Kwa wanafunzi wa Sheria hii ni kesi maarufu ya Mulbadaw. Kwa wakati huo mimi kama ilivyo wanafunzi wengine tuliichukulia kesi hiyo kama kesi ya kawaida. Ilikuwa kesi ya kufurahisha na kusisimua kama nyingine yoyote. Katika vikundi vya majadiliano na kujisomea tuliwasifia majaji kwa werevu wao wa masuala ya kisheria hasa katika tafsiri za suala la nani ni mzawa kisheria. Sikujali sana juu ya madhara ya hukumu hiyo. Kulikuwa na sababu kuu mbili au tatu, ambazo zilisababisha niwe na mtazamo au uelewa wa aina hiyo. Mosi, nikiwa mzaliwa wa Mkoa wa Ruvuma, kusini mwa Tanzania, kesi za madai ya ardhi na uhaba wa ardhi si nyingi sana ukilinganisha na sehemu nyingine. Hivyo nimejengeka kukosa mwamko wa masuala ya ardhi.

Lakini la pili ni muundo na mfumo wa elimu katika vyuo vyetu vya elimu ya juu na hasa vyuo vikuu, haumfundishi kijana kuwa mchunguzi makini na mtambuzi wa masuala ya jamii husika bali unalenga zaidi katika kazi ya kitaaluma na kufaulu mitihani. Hivyo, mtazamo wangu juu ya masuala ya ardhi, haswa suala la Mulbadaw, haukubadilika mpaka tarehe 17 Februari mwaka huu 2004 nilipopata fursa ya kutembelea eneo husika la mgogoro huo uliozungumziwa katika kesi hiyo. Mgogoro umekuwa ukiendelea kwa zaidi ya miongo 3 bila kujali hukumu ya kesi hiyo miaka kumi iliyopita. Uzoefu nilioupata, kwa kuishi kati ya wanavijiji wa vijiji saba, wengi wao wakiwa ni wale ambao walihusika kwa namna mbalimbali katika mgogoro huo umebadili mtazamo na uelewa wangu wa masuala ya Sheria na jamii.

Vijiji ambavyo nilipata bahati ya kuvitembelea ni pamoja na Mulbadaw, Bassotu, Gawidu, Laghanga, Ming'enyi na Gehandu. Vijiji hivi vimekaliwa zaidi na jamii za kifugaji hasa Wabarbaig na wakulima ambao ni Wairaqw. Makabila mengine ambayo yamehamia katika maeneo hayo miaka ya hivi karibuni ni pamoja na Wanyaturu na Wanyiramba. Shughuli hizi za ukulima na ufugaji zinawafanya wanakijiji hao waitegemee ardhi kuliko kitu kingine chochote na hivyo kuifanya ardhi kuwa kama mishipa, damu na moyo wa jamii.

Bahati mbaya, wanakijiji hawa walinyang'anywa ardhi yao na NAFCO kwa kisingizio cha Maendeleo ya Taifa.



*Immanuel Mvulla (kushoto) akifanya mahojiano na wananchi wa Hanang, kijiji cha Ming'enyi wakati wa utafiti wa HAKIARDHI.*

Unyang'anyi huu ulifanywa kikatili na kwa namna ya kushusha utu. Wakati wa kuwahamisha na miaka iliyofuata wanakijiji waliishi kama jehanamu. Kama inavyosomeka katika hukumu "uharibifu wa mali uliofanywa na mrufani" una maana tofauti sana kati ya mwananchi/mwanakijiji wa huko na mwanafunzi wa Sheria chuo kikuu. Alipoulizwa nini kilitokea

Endelea Uk. 8

# BUNGA BONGO
# Uthamanishaji wa rasilimali

*Ni jioni moja kabla ya mkutano mkuu wa wanachama na wadau wa HAKIARDHI. Baadhi ya wanachama wanakusanyika pamoja katika ukumbi mdogo wa hoteli ya Belinda, Dar es Salaam. Wanaambizana ingekuwa vizuri endapo wataongelea suala mojawapo lenye manufaa fulani (kubunga bongo) Wanakubaliana kuliongelea suala la Uthamanishaji wa rasilimali: Namna ya kuondoa umaskini kwa kutumia ardhi. Wanakubaliana, wanaanza. Prof. Chachage S. Chachage anaamua kwamba yeye atakuwa anarekodi na kunukuu. Mazungumzo yanaenda kama ifuatavyo:*

**Mzungumzaji 1:**

Umilikaji wa ardhi wa kiafrika haufai, na unarudisha maendeleo nyuma. Hivyo, Afrika nzima kumekuwa na tume za suala la umilikaji wa ardhi: Msukumo umetokea wapi? Ukibadili mfumo wa umilikaji ardhi, je kuna uhakika gani kwa wazalishaji wadogo. Mawazo mawili: Kwa hati, na wengine wanasema hata hati hazina uhakika.

Je, suala hili liko nje ya mabadiliko ya mfumo katika ujamaa kuendeleza ubepari? Kuna dhana sasa kwamba mfumo wa kibepari unaweza kuwafaidisha watu wote lakini je, huu mfumo unawajali vipi wadogo? Suala watakaloongelea wenzangu ni uthamanishaji wa ardhi: Je ina thamani gani: Na je kila mtu anaiangalia thamani kwa mwelekeo mmoja?

**Mzungumzaji 2**

Utangulizi huu watu wa kijijini wangeweza wasiuelewe, kwani watu hawaongelei juu ya ardhi. Ardhi ni kama vile maji au hewa. Leo hii hili suala linaongelewa kwa sababu ya Maendeleo yaliyotokea (elimu, teknologia, sayansi n.k.) Zamani watu huishi tu - Watu waliamini kwamba wote wamezaliwa juu ya ardhi, na kila kitu kinachotokana na ardhi ni halali yao. Hivyo ardhi ni ya kila mtu.

Maisha yana uhusiano mkubwa na ardhi na thamani yake ni kile kinachovunwa. Vyakula vya asili: Kikukwe, kumra, saga, mboga zilichumwa na watu porini. Hawakulima mboga. Kila kitu kilikuwa ni cha wote. Hata katika ufugaji, iliwezekana mtu kuhama na mifugo yake kutafuta machunga mazuri. Ukitaka ardhi unaitumia. Watu walionyesha kumiliki ardhi kwa kukata mti - tayari alama kwamba una haki ya kulima pale. Kama mwakani hulimi, mtu halimi. Lakini kukiwa hakuna dalili ya kulima, basi mwingine aliingia kulima.

Maendeleo yamebadilisha hayo, mgawanyo wa kazi na watu kuishi kwa kutegemea vitu vingine zaidi ya ardhi.

Mazungumzo ya sasa hivi yanahusu kubadilisha mfumo ili ulingane na mabadiliko hayo. Sasa nia ni kuingiza mfumo tofauti. Badala ya kuwa ni ya wote, sasa inakuwa ni ya watu binafsi (freehold or leasehold). Ardhi haisaidii bila kuwa na thamani. Hivyo unaweza ukaiuza ukapata fedha, ukapata vitu vingine unavyovihitaji. Uwezekano wa kuifanyia ardhi biashara. Hivyo inabidi iwe ni ya mtu binafsi. Mjadala ni: Je tunataka ardhi iwe bidhaa ambayo unaweza ukaiuza au ukaikopea? Au ardhi ibakie kama zamani - kwamba haina thamani. Wanasema ardhi ikibadilishwa, basi ndio mwanzo wa kufuta umaskini, kwani unaweza ukakopa na kufanya shughuli zingine ambazo zitakupa faida, itakayokuwezesha kulipa, ukishindwa kulipa, basi inabidi unyang'anywe ardhi.

Je, tunataka ardhi iweze kufanyiwa biashara? Mtu akija akasema "nipe hela" unamwuliza " na wewe utanipa nini? Ng'ombe, mbuzi ama ardhi?" Hatari sasa ni pale utakaposhindwa kulipa. Kila atakayeshindwa, benki inachukuwa ardhi yake mwishowe ardhi yote inaondoka. Na tukiendelea kukopa hivi, Tanzania sasa ina deni la shillingi billioni takriban 8 na imeshindwa kulipa. Baadae na watanzania wote tutakuwa na madeni. Je hii itakuwa busara kweli?

**Mzungumzaji 3**

Nini maana ya kuipa thamani ardhi? Leo kikubwa ni kuthamanisha ardhi na hata mali ya maskini ili kuondoa umaskini. Je maana yake ni kwamba ardhi haikuwa na thamani hapo awali? Je mkulima hapo awali hakujua kama ardhi ina thamani? Thamani ya kila kitu ni ile 'use value' (thamani matumizi) kama faida, chakula n.k.. Kinachozungumziwa hapa ni ile exchange value (thamani soko). Nitumie mfano mmoja: Mtoto akienda dukani kununua pipi anaiona ile pipi ina thamani kubwa kwake. Na thamani yake ni kujiburudisha. Lakini thamani ya pipi kwa mwenye duka si kuburudisha, bali kuweza kuiuza. Lakini kila mmoja kati yao anaipa pipi thamani kulingana na nia



*Wakurugenzi wa HAKIARDHI wakijadili jambo. Kutoka kulia ni Issa Shivji, Wilbert Kapinga na Ng'wanza Kamata (Mkurugenzi Mtendaji)*

yake. Thamani soko inatambua umilikaji na ulinzi wa milki. Kuna uhusiano kati ya mtu na kitu. Uhusiano uliopo ni kwamba kama mimi nina haki hapa, basi wewe huna haki: Maana halisi ya umiliki unaozungumziwa ni uhodhi. Na kuifanya hivyo, si kwa kila mtu, bali kwa watu wachache, na wengine wasiwe nayo.

Walowezi katika uchumi wa kikoloni huko Kenya na Zimbabwe, walihodhisha ardhi kwa wazungu wachache ili wenyeji wasiwe na ardhi ili wawe wafanyakazi wa wazungu. Hivyo unahodhisha na kumilikisha. Thamani soko maana yake ardhi iwe bidhaa - inunuliwe na kuuzwa. Lakini huwezi ukaipeleka sokoni. Hivyo lazima utenganishe matumizi ya ardhi na umilikaji. Mtumiaji anaweza asiwe mmilikaji. Utenganishwaji unafanywa hivyo kwa njia ya hati miliki. Ndiyo maana ya ardhi kuwa bidhaa.

Maana halisi ya kuthamanisha ardhi - ili iwe na manufaa kwa maskini: je wakishindwa kulipa? Lakini hoja inajengwa kwa madai ya kutaka kuwaendeleza - ati wana ardhi lakini hawataki kuitumia. Je hii ni kweli? Asilimia 80 ya watanzania ni wakulima - kutoka ekari 1-4-6-10 au 12. Benki gani ya kibiashara itachukuwa ardhi kama hiyo?

Hakuna benki ya biashara inaweza kuchukua ardhi kama hiyo, au kumpa mkopo mkulima mdogo huyo. Mahali popote wakulima wamekuwa wakipewa mikopo na serikali au ushirika (floating charges) wakaweka rehani mazao yao na si ardhi yao.

Sasa kwa nini leo kung'ang'ania ardhi ambayo ndiyo maliasili ya mwisho waliyobaki nayo? Ukweli ni kwamba hao wawekezaji wanatafutiwa ardhi na TIC na baada ya kupata hati miliki ya 50,000 ha. anadai kwamba ana capital ya kiasi fulani anachukuwa hati miliki na kuipeleka Standard Chartered au NBC na kuchukuwa mkopo. Haingizi nchini hata senti moja. Mkopo anaoupata ni malimbikizo ya watanzania maskini. Hizo ndizo atawekeza miaka mitano halipi kodi. Halafu anafanya kazi kwa miaka 4 na kudai kwamba alipata hasara ili apewe tena miaka 5 zaidi ya bila kodi. Hivyo ndivyo ilivyo.

Sasa vipi huo mfumo unaondoa umaskini? Ni wazi kabisa kwamba huu mfumo unaendeleza umaskini: Suala la muhimu ni namna gani unaweza kusaidia hohehahe?

Nadhani kuna haja ya kuelewa kwa undani zaidi:

**Nini maana hasa ya kuthamanisha ardhi?**

**Mzungumzaji 4**

Tupende tusipende hao wawekezaji wanakuja. Kila mkoa umeorodhesha ardhi ambayo inafaa kwa kilimo lakini "isiyotumika". Hiyo ndiyo ardhi wanayopewa wawekezaji. Hii ndiyo biashara. Akisema anataka ekari 5000 huko Kilimanjaro, wanamwambia " Samahani bwana, huko hatuna lakini tunaweza kukupatia Bukoba kama utapenda?".

Kama wawekezaji wanashughulikiwa hivyo, hao wanavijiji kwa nini hawashughulikiwi?

**Mzungumzaji 5**

Haya ni mambo ya msingi ambayo yanaweza kutuletea matatizo makubwa. Mfano vijiji vya Ujamaa. Tulilazimishwa kuingia huko bila ridhaa yetu lakini baadae tukakubali kwa ahadi za kutokusumbuliwa. Lakini sasa tumeondolewa kwa nguvu na hatuna pa kulima. Tutaishi vipi? Tukikaa mijini tunaambiwa tunaleta msongamano, tukienda pembezoni tunafuatwa na kunyang'anywa mashamba. Tanzania sasa inaingizwa katika mikataba ya hiari ili baadae tuje kukwama halafu waendelee kututawala. Hawa wawekezaji wanang'ang'ania ardhi kwa vile inaongezeka thamani kila siku.

**Mzungumzaji 6**

Walaji ni wengi sana. Kuanzia wadogo wadogo, wa kati na wa juu kabisa. Hata sisi wasomi (Maprofesa) tunakula. Kila mtu anakula kwa nafasi yake. Kila mbuzi na kamba yake.

Ukitazama kihistoria, wimbi la kwanza la ugomvi wa ardhi ni wakati wa ukoloni. Wengine walikuja kama walowezi wengine wakasema tuzalishe kwa ajili ya soko la dunia. Hata kwenye miaka ya 50 haya tunayozungumzia leo yalishapamba moto wakati watu walipoanza kudai mfumo wa ardhi ubadilishwe. Mambo ya "freehold" yalianza ili kuwamilikisha waswahili wachache waanze kulifaidi hilo soko. Mambo ya utaifishaji nayo yakaja miaka ya 70 duniani kote. Ardhi si sera peke yake ambayo imekumbwa na mambo haya. Nchi zilizoendelea ziliweka masharti ambayo yaliingilia sera za ndani za nchi zinazoendelea. Sera zilizowekwa hazikuwajumuisha wakulima na wafugaji. Ilikuwa ni "partnership ya makundi manne: Serikali, donor, sekta binafsi na NGO.

Wafanyakazi na wakulima hawapo popote. Wao wanaonekana wavivu, maskini na wasiopenda maendeleo. Eti "Mtaji wa maskini ni nguvu zake mwenyewe" Hatuangalii kama hawa watu wamenyang'anywa ardhi, hawana vitendea kazi ama pembejeo. Mimi nasema "Utajiri wa tajiri ni nguvu za maskini!" Hata huko Mexico mwaka 1994 walipoambiwa kuhusu soko huria la ardhi wakasema, bwana, huu mfumo nia yake ni kutunyanganya haki wenyeji na kufanya ardhi yetu ichukuliwe na wageni. Tunachojua sisi ni haki na misingi ya uwezo ili watu waweze kujikimu. Kinachogomba ni jinsi ya kuendelea na kuwa na maisha bora na sio jinsi ya kumiliki ardhi.

*Mjadala huu uliwahusisha watu wenye ufahamu wa juu kuhusu sera za ardhi na mabadiliko yake. Natumaini pia wewe ungekuwepo ungetoa mchango wako. Tutumie maoni yako ili tuendeleze mjadala.*

# UHABA

*Inatoka uk. 5*

baada ya NAFCO kuwasili, bibi mmoja alikuwa na haya ya kusema: "Hakuna jambo baya au bovu duniani ambalo NAFCO haijatutendea" Kwa kisingizio cha Maendeleo ya Taifa, wanakijiji wakaitwa si wazawa, mali zao zikaharibiwa na pia hitaji la kuleta askari wa kikosi cha kutuliza ghasia (FFU) ili kuzima "uasi" wa wanavijiji au "wasio wazawa" (Ukipenda kuwaita) ukafanywa. Hawa wasio wazawa wakasukumwa kwenye maeneo yasiyo na rutuba, yenye mawe, changarawe na kokoto katika kingo za bonde la ufa na hivyo kuunda vijiji saba. Utazamapo uwanda wa bonde la ufa kutoka katika mojawapo ya vijiji hivi utaona ardhi murua yenye rutuba ambayo ipo chini ya PSRC tayari kwa kupigwa mnada. Kama ulikuwa na tabasamu, basi linatoweka pale ukumbukapo kwamba kuna watu wasio na ardhi waishio kati ya ardhi tele yenye rutuba nzuri lakini wasiyoweza kuitumia.

"Tuna tatizo kubwa la ardhi" anasema Jonathan Afisa Mtendaji wa Kata ya Bassotu "Familia inaweza kuwa na wastani wa eka tatu tu za ardhi. Hii haikidhi kabisa mahitaji ya familia nzima ukilinganisha na ukubwa wa familia na mifugo kati ya wafugaji."

Uongozi wa Kijiji kwa mfano, unapokea malalamiko mengi yatokanayo na ardhi. Migogoro kama ile ya mipaka, kulima kwenye *mapario* (barabara za kupitishia ng'ombe) na hata migogoro inayosababishwa na wahamiaji. Ukweli ni kwamba idadi ya wanakijiji inaongezeka wakati ardhi inabaki kuwa ile ile. Katika vijiji vyote nilivyotembelea wenyeviti wa vijiji wamekiri na kuthibitisha kuwa hakuna ardhi tena kwa ajili ya wanavijiji wapya. "Tunawahimiza wahamie mikoa yenye ardhi au watumie ardhi ya familia. Hatujagawa ardhi kwa zaidi ya miaka mitatu sasa kwa yeyote na idadi ya wasio na ardhi inaongezeka." Anasema mwenyekiti wa kijiji cha Dang'aida. "Idadi ya waliojiandikisha kwa ajili ya kugawiwa ardhi inaongezeka ukitilia maanani idadi ya vijana wanaomaliza shule." Anaendelea kueleza mwenyekiti huyo.

Mbinu inayotumika kama sulihisho la kupunguza ukali wa tatizo ni kukodi au kuazima shamba. Gharama ya ekari moja ni kati ya T.Shs.5,000 hadi 10,000 kwa msimu mmoja wa kilimo. Hili nalo linaathari zake: anayekodi hawezi kuwa na uhakika wa kulitumia shamba hilo kwa muda mrefu. Pili hupata hasara endapo, kutakuwa na uhaba wa mvua hivyo kukosa mavuno. Lakini pia mtindo huu hauwafai wafugaji kwani ardhi wanayohitaji ni kubwa zaidi hivyo kushindwa kukodi.

Kama ilivyo katika sehemu vyingi za Tanzania mwaka huu, eneo hili nalo limekumbwa na baa kubwa la njaa. Hali za maisha za wananchi zilikuwa duni na kwa kweli zilitia simanzi. Kina mama na watoto walionekana wakiokoteza punje za mahindi sokoni na kuzila vivyo hivyo. Huzuni na simanzi za hali ile zilifanya baadhi yetu kushindwa kuzuia machozi kutudondoka. Japo hali hii ya uhaba wa chakula yawezekana imechangiwa na uhaba wa mvua, suala la ukosefu wa ardhi linabaki kuwa kinara. "Huwezi kudanganya kwamba njaa hii inasababishwa na ukosefu wa mvua pekee, kama watu hawatapata ardhi ya kutosha hali hii itaendelea kila mwaka", alisisitiza kiongozi mmoja wa kimila. Lakini pia katika kuokoa maisha ya watu walio katika njaa serikali haikutoa misaada ya kutosheleza mahitaji ya karibu kaya 400 kila kijiji. Watoto walikuwa wakiteseka na njaa wakati wale waliosababisha kuwepo kwa hali hiyo wakila na kusaza.

Siku kumi za kuwa Hanang zilikuwa hazijaisha, na katika kipindi hicho nilibaini kuwa chanzo cha matatizo mengi ya eneo hilo ni NAFCO. Iwe ni njaa, umaskini au migogoro ilikuwa ina uhusiano wa namna moja au nyingine na uanzishwaji wake. Hii ni ardhi ambayo watu walinyang'anywa na kwa sasa matumizi yake yamefikia ukomo. Sababu za kufa kwa NAFCO haziko wazi, pengine ni hali ya hewa, soko huria au uongozi mbovu. Hizi ni sababu ambazo hazitoshelezi uelewa wa mwananchi wa kawaida ambaye ana uhaba wa ardhi. Kinachoendelea juu ya ardhi hiyo ni PSRC tu wanaokifahamu. Wanavijiji wa Hanang hawaifahamu PSRC ama mipango inayoendelea kuhusu NAFCO.



***Baadhi ya wananchi katika kijiji cha Ming'enyi wakisubiri kugawiwa mahindi ya msaada***

"Hatujui kilichoipata NAFCO na wala hatutaki kujua. Tunachojua ni kwamba tunahitaji kurudishiwa ardhi yetu kwa manufaa yetu na watoto wetu". Walisema wazee wa kimila, sentensi ambayo iliniingia vilivyo na kunifanya nielewe vyema usemi wa uhaba palipo na tele.

# KIGAMBONI WALALAMIKIA NA KUHOJI UPORAJI WA ARDHI

*Na Mwandishi wetu*

Uporaji wa ardhi ya wakulima wakazi wa eneo la Kigamboni, Wilaya ya Temeke Mkoani Dar es Salaam umelalamikiwa na wananchi. Malalamiko hayo yalitolewa kwenye semina iliyofanyika tarehe 03/04/2004 katika kijiji cha Buyuni, Kata ya Pemba Mnazi Wilayani Temeke. Katika semina hiyo, iliyoshirikisha wakazi wa vijiji vya Buyuni, Pemba Mnazi, Mwongozo na Kimbiji ilielezwa kwamba wananchi wamekuwa wakipoteza ardhi yao ama kwa ulaghai au vitisho vinavyotolewa na viongozi wao. Aghalabu ulaghai au vitisho hivyo vimetolewa ili kukidhi maslahi ya matajiri wenye nia ya kuhodhi maeneo makubwa katika eneo hilo la pwani. Pia ilibainika kuwa ulaghai na vitisho hivyo huambatana na upindaji na ukiukaji wa makusudi wa Sheria za ardhi na taratibu za utwaaji wa ardhi kwa mujibu wa Sheria za ardhi hususan Sheria ya Utwaaji Ardhi ya Mwaka 1967. Washiriki katika semina hii walitahadharisha kuwa uporaji huu haupaswi kuendelea kwa sababu siyo tu unawasababishia matatizo makubwa bali pia unawafukarisha. Rai yao kwa serikali na wawakilishi wao ni kuwa wazingatie na kuheshimu taratibu na Sheria zinazoongoza utwaaji ardhi pale inapokuwa lazima ardhi katika eneo lao kutwaliwa na kuwashirikisha kikamilifu wananchi. Aidha, walisisitiza kuwa viongozi katika maeneo yao waache uwakala wa kuuza haki zao za ardhi kwa niaba ya matajiri na wanasiasa.

Wakati huo huo, Taasisi ya HAKIARDHI iliwaeleza wananchi hao vipengele muhimu vinavyojitokeza katika Sheria ambavyo vitawasaidia katika kutatua migogoro miongoni mwao na kufahamu haki zao na namna ya kujilinda na ubadhirifu wa wananchi wenye tamaa ya kujilimbikizia ardhi kubwa. Waendesha warsha pia walielezea kwa ufupi mabadiliko ya Sheria ya ardhi ya mwaka 2004 na kuonya kuhusu madhara ambayo yanaweza kujitokeza endapo wananchi hawatakuwa makini.



*Washiriki wa moja ya semina za HAKIARDHI wakifuatilia jambo kutoka kwa Rehema Mfaume (kushoto). Katikati ni Subira Kibiga (mwanachama wa HAKIARDHI) na kulia ni Rehema Kerefu (Mwezeshaji).*

# HANANG

*Inatoka uk. 4*

kutegemea mvua, ni ardhi ya kutosha kwa ajili ya shughuli zao za kilimo na ufugaji. Kwa upande wao wananchi, hasa kinamama wa maeneo haya wanatoa rai kwa serikali kurejesha mashamba haya kwao - wananchi.

"Hakuna asiyejua umuhimu wa ardhi", alibainisha mama mmoja, "ardhi ndiyo tegemeo la maisha yetu sote wake kwa waume." Lakini kwa nini wananchi na akina mama hawa wadai kurejeshewa ardhi yalipo mashamba ya NAFCO leo? Jibu lao ni kuwa ardhi waliyonayo haitoshi, na NAFCO ilivyochukua ardhi yao miaka ya 1970 ndiyo ililikuza tatizo hilo kwa sababu maeneo ya kulisha mifugo yalipungua na kuathiri sana mifugo na maisha yao. "Tungependa kuona ardhi hii iliyokuwa mashamba ya NAFCO ikirejeshwa kwetu", alisema mwanamke mwingine, "sisi tumezaa na watoto wetu wanahitaji ardhi kwa ajili ya maisha yao".

Japokuwa kilimo na ufugaji kinategemea kwa kiasi kikubwa msimu wa mvua na upatikanaji wake, ni dhahiri kuwa bila ardhi hata kama kungenyesha mvua ya kutosha na kwa wakati unaotakiwa bado wakazi hawa wasingekuwa na uhakika wa chakula. Wanawake na wanaume wa Hanang wanakiri kuwa ipo haja ya kilimo na ufugaji wao kuboreshwa zaidi lakini hii haifuti ukweli kuwa ardhi waliyonayo haitoshi na wanahitaji ardhi zaidi kuendesha maisha yao na ya watoto wao. Aidha ni wazi kuwa kuwepo kwa wakulima wakubwa miongoni mwao hawakuona kama ni jambo lenye manufaa au heri yoyote. Kumbukizi za NAFCO na himaya yake zinaonesha kuwa ukulima wa mashamba makubwa haulengi kuwanufaisha wakulima na wazalishaji wengine wadogo wadogo waishio jirani. Endapo chini ya NAFCO, shirika la umma, umma wa wanavijiji wa Hanang uliathirika na kuhasirika badala ya kufaidika itakuwaje chini ya mtu binafsi mwenyeji au mgeni tajiri, je mambo yatakuwa tofauti? Kinamama wa vijiji kuzunguka mashamba yaliyofilisika ya NAFCO wilayani Hanang wanaonesha hofu na wasiwasi wa dhahiri. Wanaona shari mpya inawakaribia ambayo yawezekana ikatonesha majeraha yao yaliyotokana na kuundwa NAFCO hapo awali.

**"Hakimu mwema hachelei macho ya mtu mwingine kutazama hukumu aliyotangaza kuwa haki" (Shaaban Robert 1966).**

# Maoni ya Wananchi kuhusu mabadiliko ya sheria ya ardhi



Na Agripina Habicht

***Hivi karibuni Bunge lilijadili na kupitisha mabadiliko ya sheria ya Ardhi hususan kuhusiana na kuipa dhamani, kuweka rehani na kuuza ardhi na mambo mengine. Haya ni mabadiliko makubwa sana katika sheria hii ambayo yanaweza kuleta athari kubwa kwa wananchi hasa wale waishio vijijini. Maoni mengi yelitolewa na wananchi kupinga baadhi ya vipengele vilivyopitishwa kwa hofu ya kuwaletea ufukara watanzania na hata kuwafanya watumwa wa matajiri watakaonunua sehemu kubwa ya ardhi ya nchi hii. HAKIARDHI imechambua baadhi ya maoni yaliyotolewa na wananchi baada ya mabadiliko hayo kupitishwa:***

### Hakuna haja ya kubinafsisha ardhi

**Ponsian Rwechungura: *Mwananchi, Aprili 16 2004***

Mabadiliko ya sheria ya ardhi yanaendeshwa kwa nia mbaya ya kuwapora mashamba Watanzania ili wakishindwa kurejesha mikopo, mashamba yao yapigwe mnada. Wafanyabiashara wenye hila watatumia nafasi hiyo kujineemesha kupitia migongo ya walalahoi. Hakuna haja ya kubinafsisha ardhi kwa sababu bado Watanzania wengi hawajajiandaa vya kutosha kushindana katika biashara na wageni kutoka nje.

Kwa utaratibu unaozungumzwa katika sheria ingepaswa kuangalia masuala yafuatayo: Ukweli kwamba watanzania wengi hawatumii mabenki, hawajafahamishwa vya kutosha kuhusu shughuli zake, faida na hatari za kukopa kwa ajili ya biashara. Jambo jingine ni kwamba wananchi ambao wanaishi vijijini hawana mali wanayoweza kuweka kama dhamana kupata mikopo. Ardhi ambayo ni mali pekee ikichukuliwa au kuwekwa rehani wananchi hao wataendelea kuwa maskini.

### Sheria za ardhi hazilindi haki za wapangaji na wenye nyumba.

**Ludger Nyoni: Mtanzania, *Machi 30, 2004***

Sheria mpya ya Mabaraza ya Ardhi na Nyumba ya Wilaya na Mahakama Kuu ya Ardhi haina vifungu vyovyote vinavyoonyesha wazi kwamba vimewekwa kwa kulinda haki za wapangaji na wenye nyumba. Inasikitisha kuona Wizara imefanikiwa kulishauri Bunge letu kupitisha sheria ya ukandamizaji wa wapangaji. Kitendo cha kuyaondoa mabaraza ya nyumba ya Mikoa na Baraza la Rufaa ni dalili ya wazi ya ukandamizaji kwa wapangaji na kinapaswa kilaumiwe na kila Mtanzania mpenda haki na jumuiya ya kimataifa. Jambo la kusikitisha zaidi ni kwamba sheria hii mpya ya Land Disputes Courts Act No. 2 ya 2002 imepitishwa bila ya kushirikishwa wapangaji au chama chao na wenye nyumba kutoa maoni yao na huo siyo ustaarabu kwa dunia hii ya leo ya utandawazi.

### Tanzania tufuate nyayo za Mugabe

**John J. Ayo: Rai, *Machi 4-10, 2004***

Serikali ya Tanzania imemsifu na kumuunga mkono Rais Mugabe wa Zimbabwe kwa hatua yake ya kijasiri ya kuwanyang'anya walowezi mashamba yake na kuwapa wananchi wake. Mimi namuunga mkono rais Mugabe, lakini alichelewa kidogo kuwatimua walowezi hao ndiyo maana sasa hivi hatua yake hiyo inampa taabu kidogo.

Tanzania tunajifunza nini kwa Mugabe? Mwalimu hakuweka ardhi ya Tanzania "poni" (rehani). Aliacha kila kitu safi kabisa lakini sasa ardhi ya Tanzania imewekwa poni. Nasema hivyo kwa sababu mbali na wakubwa kuwa ndio wamekuwa walowezi kwa kuchukuwa ardhi nzuri, tumekaribisha wageni kwa jina au kivuli cha uwekezaji.


Wazee wetu walipigana kwa sababu ya ardhi na ndiyo maana tuna nchi inayoitwa Tanzania. Tusome vitabu vya wanaharakati wafuatao: Earl Seaton na Kirilo Japhet- The Meru Land Case (Kesi ya Ardhi ya Meru); Ax Nelson- The Freemen of Meru (Raia Huru wa Meru); Vita ya Maji Maji, Wahehe walipigana na Wajerumani kwa sababu ya ardhi na si vinginevyo.




*Wanaharakati wakiwa wamebeba mabango kupinga kupitishwa kwa marekebisho ya sheria ya ardhi wakati yalipowakilishwa Bungeni*

# MACHAPISHO

| Na. | Jina la Kitabu | Mwandishi |
|---|---|---|
| 1. | Not Yet Democracy: *Reform land tenure in Tanzania - 1998* | Issa G. Shivji |
| 2. | Ardhi ni Uhai - *1995* | Georgios Hadjivayanis |
| 3. | Mwongozo wa Haki za Ardhi kwa Wananchi wa Tanzania - *2002* | Issa G. Shivji/ Deus Kibamba |
| 4. | Fukuto la Migogoro ya Maeneo na Hatma ya Wazalishaji Wadogo Wadogo Tanzania - *2002* | Aida Isinika (Mhariri) |
| 5. | Msukumo na Harakati za Kubadili Mfumo wa Umilikaji Ardhi Tanzania - *2000* | Ng'wanza Kamata (Mhariri) |
| 6. | Maasai Rights in Ngorongoro, Tanzania - *1998* | Issa G. Shivji & Wilbert Kapinga |
| 7. | Haki za Wamaasai waishio hifadhi ya Ngorongoro *1999* | Issa G. Shivji, Wilbert Kapinga, |
| 8. | Mfumo wa Umilikaji Ardhi Tanzania, *1997* | Issa G. Shivji and Wilbert Kapinga (Wahariri) |





*Karibuni kwenye semina zetu za kila mwezi jengo la umoja wa vijana barabara ya Morogoro. Wasiliana nasi (hasa kwa barua pepe au simu) ili tukujulishe tarehe za semina.*

HAKI ARDHI

# "RUKSA ARDHI KUUZWA KAMA KANZU!!"

HAKIARDHI



"Katika nchi kama yetu, ambamo waafrika ni masikini na wageni ni matajiri, kuna uwezekano mkubwa kwamba Mwafrika akiruhusiwa kuiuza ardhi, katika miaka themanini au miaka ijayo, ardhi yote ya Tanganyika itamilikiwa na matajiri wageni, na wenyeji watakuwa watwana. Lakini hata kama wageni wasingekuwa matajiri, litaibuka tabaka la watanganyika matajiri na wajanja. Tukiruhusu ardhi iuzwe kama kanzu, katika muda mchache, kutakuwa na kundi dogo la waafrika wakiwa na ardhi na walio wengi watakuwa watwana"

Mwl. Julius K. Nyerere, 1958

**Pamoja na kwamba Sheria ya marekebisho ya sheria ya ardhi ya 2004 imeruhusu ardhi tupu kuuzwa, Je, mambo haya aliyoyasema Mwl. Nyerere yamepitwa na wakati?**

**Anuani/Ofisi**
Taasisi ya Utafiti na utetezi wa Haki za Ardhi **(HAKIARDHI)**, Br. Morogoro , Jengo la Vijana , Chumba na. 4, Ghorofa ya mwisho. S.L.P. 75885, DSM, Tanzania. Simu/Faxi +255 22 2152448, +255 748 646 752.
E-mail: hakiardhi@raha.com/info@hakiardhi.org
Tovuti: www.hakiardhi.org

ARDHI NI UHAI